East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature

OPEN ACCESS

*Abbreviated Key Title: East African Scholars J Edu Humanit Lit*
ISSN: 2617-443X (Print) & ISSN: 2617-7250 (Online)
Published By East African Scholars Publisher, Kenya

Volume-9 | Issue-9 | Sep- 2026 | DOI: https://doi.org/10.36349/easjehl.2026.v09i09.003

Original Research Article

# Athari za Ujinsia Unaodokezwa katika Majina ya Watu ya Jamiilugha za Kibantu Nchini Tanzania

Zacharia Madila[1]*
[1]Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania

**Article History**
**Received:** 17.07.2026
**Accepted:** 01.09.2026
**Published:** 03.09.2026

**Journal homepage:** https://www.easpublisher.com

**Quick Response Code**

**Abstract:** Majina ya watu hayatumiki kama utambulisho wa watumiaji wake pekee, bali ni nyenzo inayotumiwa na wanajamii kuendeleza amali, tamaduni, historia, mamlaka, na mahusiano ya wanajamii. Makala hii imechunguza athari za ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu nchini Tanzania kwa watumiaji wa majina husika. Data za utafiti huu zilikusanywa kutoka katika jamiilugha za Kiswahili, Kinyakyusa, Kisambaa, Kigogo, Kisukuma, na Kiha katika mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Tanga, Dodoma, Mwanza, na Kigoma. Aidha, data hizo zilikusanywa kwa njia ya usaili na majadiliano katika makundi lengwa kutoka kwa watoataarifa 240 wa umri wa zaidi ya miaka 25. Kadhalika, data zilikusanywa na kuchanganuliwa kitaamuli kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa maudhui na kuongozwa na Nadharia ya Ubabedume ya Bly (1970). Kwa ujumla, imebainika kuwa athari za ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu kwa watumiaji wake ni kuwa ujinsia hujenga na kuimarisha tabia za wanajamii, huukilia mamlaka za watu katika familia na jamii, na husababisha matatizo ya kisaikolojia kwa wanajamii. Athari zingine za ujinsia ni kuwa huukilia mahusiano ya wanajamii kwa Mungu na wahenga, huukilia mafanikio ya wanajamii, hudhibiti mawanda ya upataji maarifa kwa wanajamii, na huchochea wanajamii kuchukia lugha na tamaduni zao. Hivyo basi, makala hii inatoa rai kuwa mamlaka za utoaji wa majina ya watu ziweke umuhimu mkubwa katika mchakato wa utoaji wa majina ya watoto kwani majina hayapo kwa ajili ya utambulisho pekee, bali ni nyenzo madhubuti ya kufinyanga na kuamua mwelekeo na hatma za maisha ya wanajamii na jamii kwa ujumla.

**Keywords:** Ujinsia, Ubabedume, Majina ya Watu, Jamiilugha za Kibantu.

**Copyright © 2026 The Author(s):** This is an open-access article distributed under the terms of the Creative Commons Attribution **4.0 International License (CC BY-NC 4.0)** which permits unrestricted use, distribution, and reproduction in any medium for non-commercial use provided the original author and source are credited.

## 1.0 UTANGULIZI

Jamiilugha huwekeza amali, historia, tamaduni, falsafa na itikadi katika majina ya watu na michakato ya utoaji wa majina husika (Adejare, 1992; Zawawi, 1993; na Wamitila, 1999). Wataalamu wa isimujamii wanasisitiza kuwa jina la mtu halifanyi kazi ya kumtambulisha mhusika na jamiilugha yake pekee, bali hubeba historia ya jamii husika, amali za jamii, utamaduni, na huonesha taswira yake (Abdul, 2013; John, 2016; Buberwa, 2018a; Lusekelo na Mtenga, 2020; Buberwa, 2022; na Bichwa, 2025). Aidha, jina la mtu ni kielelezo cha msingi kinachoweka wazi matarajio, imani, mazingira, maumbile, mahusiano, majukumu, shughuli za uzalishaji mali, na kiwango cha maendeleo yaliyofikiwa katika familia na jamii kwa ujumla (Rubanza, 2000; Nyangaywa, 2013; Buberwa, 2018a&b; na Lusekelo na Mtenga, 2020). Pia, majina ya watu ni nyenzo inayoonesha mahusiano ya kijinsia yaliyopo kati ya wanaume na wanawake katika jamiilugha husika (Buberwa, 2018a; Wappa na Wada, 2019; Mensah, 2023; na Formato na Somma, 2023).

Kadhalika, Mensah (2023) anaeleza kuwa majina ya watu hufungamana na lugha na tamaduni ambazo huaminika kuwa na msukumo katika maisha ya wanajamii. Mensah anasisitiza kuwa, majina ya watu hufasili tabia na maendeleo ya kisaikolojia ya wenye majina husika. Kwa mantiki hiyo, vipengele vya kijamii na kiutamaduni vilivyofumbatwa katika majina ya watu huwaathiri wanajamii kwa kuamua hatma za maisha yao. Kadhalika, Pilcher (2017) anaeleza kuwa michakato ya uteuzi wa majina ya watu si sawa kati ya uteuzi wa majina ya wanaume na majina ya wanawake na huzalisha na kuendeleza ubaguzi wa kijinsia. Nao, Buberwa (2018a&b), Salihu (2014), Kones na wenzie (2022), Wanyama (2022), na Formato na Somma (2023) wanaeleza kuwa mila na desturi zinazojenga na kuendeleza ubaguzi wa kjinsia hulenga kujenga na

***Corresponding Author:** Zacharia Madila
Mhadhiri Msaidizi, Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Mtakatifu Agustino cha Tanzania

kuendeleza sifa njema za mtoto wa kiume huku zikilenga kubomoa sifa za mtoto wa kike. Ni katika mazingira hayo makala hii imeangazia athari za ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu nchini Tanzania kwa wanajamii. Kwa kufanya hivyo, makala hii imeonesha umuhimu wa wanajamii kuuona mchakato wa utoaji wa majina ya watoto kama mchakato muhimu unaoamua hatma za watoto na jamii kwa ujumla.

## 2.0 METHODOLOJIA ZA UTAFITI

Data za utafiti huu zilikusanywa kutoka uwandani ambapo watoataarifa kutoka katika jamiilugha sita za Tanzania wlihusishwa. Jamiilugha hizo ni Wasukuma, Waswahili, Wasambaa, Wanyakyusa, Wagogo, na Waha. Jamiilugha hizo ziliteuliwa kinasibu ili kuwakilisha mikoa na kanda za Tanzania ambapo Wasukuma wa Mwanza kwa Kanda ya Ziwa, Wagogo wa Dodoma kwa Kanda ya Kati, Wasambaa wa Tanga kwa Kanda ya Kaskazini, Wanyakyusa wa Mbeya kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Waswahili wa Dar es Salaam kwa Kanda ya Pwani, na Waha wa Kigoma kwa Kanda ya Magharibi. Aidha, jamiilugha teule zinawakilisha makundi sita ya lugha za Kibantu kama yalivyoainishwa na Maho (2014) ampapo lugha hizo zimepewa misimbo ifuatayo: Kiswahili (G40), Kiha (D66(J)), Kisukuma (F21), Kisambaa (G23), Kinyakyusa (M31), na Kigogo (G11). Hivyo basi, makundi hayo yanatoa uwakilishi wa jamiilugha za Kibantu. Kwa kushughulikia makundi yote ya jamiilugha za Kibantu kwa uwakilishi sawa yamepatikana matokeo jumuishi kuhusu athari za ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu kwa watumiaji wake.

Kadhalika, data za makala hii zilikusanywa kutoka kwa watoataarifa 240 wa umri za zaidi ya miaka 25 kwa njia ya usaili na majadiliano katika makundi lengwa. Hivyo basi, jumla ya watoataarifa 40, 20 wanaume na 20 wanawake, kutoka katika kila jamiilugha walipatikana katika kata mbili za maeneo teule. Kata ya Goba na Manzese za Wilaya ya Ubungo Mkoani Dar es Salaam, Lusungo na Bondeni za Wilaya ya Kyela Mkoani Mbeya, Malya na Hungumalwa za Wilaya ya Kwimba Mkoani Mwanza, Kigondo na Msambara za Wilaya ya Kasulu Mkoani Kigoma, Chali na Bahi za Wilaya ya Bahi Mkoani Dodoma, na Bungu na Makuyuni za Wilaya ya Korogwe Mkoani Tanga. Pia, mbinu ya usampulishaji nasibu tabakishi ilitumika katika uteuzi wa tabaka la watoataarifa wa umri wa zaidi ya miaka 25. Aidha, mbinu ya usampulishaji fursa ilitumika katika kuteua wanajamii kwa ajili ya usaili na majadiliano katika makundi lengwa. mtafiti alianza kwa kumsaili mtoataarifa mmojammoja kisha kuandaa majadiliano katika makundi ili kupata picha pana zaidi ya kijamii kuhusu athari za ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu kwa watumiaji wa majina husika. Kwa hiyo, mtafiti alimhusisha kila mwanajamii aliyejitokeza na mwenye sifa na nafasi ya kutoa taarifa kwa ajili ya utafiti huu.

Vilevile, mtafiti aliomba vibali vya utafiti kutoka katika mamlaka za maeneo teule. Pia, mtafiti aliwafahamisha watoataarifa wake kuwa kushiriki katika utafiti huu ni hiari na taarifa watakazozitoa zitatumika kwa ajili ya utafiti pekee. Zaidi ya hayo, uchanganuzi wa data umefanywa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli kwani data zilikusanywa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Faukwa ya hayo, data hizo zilichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa maudhui. Mbinu ya uchanganuzi wa maudhui imetumika katika makala hii kwa kuwa hushughulikia maudhui katika matini na uhusiano wake. Hivyo basi, suala la ujinsia katika majina ya watu na uhusiano wake na hatma za wanajamii na jamii kwa ujumla limechunguzwa kwa kuchanganua maudhui ya taarifa zinazohusu athari za ujinsia unaodokezwa katika majina ya jamiilugha za Kibantu kwa wanajamii.

## 3.0 KIUNZI CHA NADHARIA

Uchanganuzi wa data za makala hii umeongozwa na Nadharia ya Ubabedume ya Bly (1970). Misingi ya Nadharia ya Ubabedume inaeleza kuwa, kwanza, utawala wa wanaume umehalalishwa katika kila sehemu ya maisha kwa kusisitiza maumbo ya vitambulishi vya jinsia ya kiume kwa misingi ya jamii, maandishi, na matukio au maelezo ya kihistoria. Pili, wanaume wametawala na kuwa na mamlaka makuu katika jamii kwa kushikilia nafasi na rasilimali zenye thamani katika jamii kama vile kazi, pesa, na taasisi za kijamii zenye nguvu kama serikali na dini. Tatu, desturi za jinsia ya kiume zimehalalishwa kwa madai kuwa wanaume wengi husukumwa kutenda kulingana na ubabedume. Aidha, lazima mwanaume awe mshindi katika hali zinazohitaji nguvu za kimwili, na awe na uwezo wa kuamua na kufikiri kiurazini. Nne, kutokana na mabadiliko na changamoto katika jamii, mgawanyo wa majukumu ya kiutamaduni kijinsia hauna nafasi katika ulimwengu wa sasa.

Tano, wanaume wameweka utambulisho wao katika sura na mfano wa Mungu kwa manufaa yao wakizingatia kwamba mwanaume alipewa mwanamke kama mwenzi kutoka kwa Mungu ambaye ni wa kiume. Sita, wasiwasi unaowakumba wanaume kwa kupoteza heshima na ubainifu wa majukumu yao ni halali. Mwisho, Nadharia ya Ubabedume inadai kuwa maeneo ya ubabedume hujitokeza katika desturi kwa ujumla kupitia maumbile, nguvu za kimwili, ushujaa, kufanya kazi, kukidhi mahitaji ya familia, kuwa na tajriba ya shari ya kijinsia, ukakamavu, urazini, kutaka makuu, majivuno, uadilifu, ushindani, na kuthubutu mambo. Kwa hiyo, misingi yote ya nadharia imetumika katika makala hii kwa sababu athari za ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu kwa watumiaji wake ni suala la kiutamaduni linalohusisha mahusiano ya wanaume na wanawake wa jamiilugha husika. Aidha, ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu umejengwa katika misingi ya mfumodume inayowapendelea zaidi watoto wa kiume kuliko watoto wa kike. Kwa mantiki hiyo, athari za ujinsia

unaodokezwa katika majina ya watu zimekaa kitabaka ambapo hulenga kuendeleza utawala wa wanaume huku zikilenga kuwakandamiza wanawake. Hivyo basi, mtafiti amechunguza athari za ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu nchini Tanzania kwa watumiaji wake. Kwa ujumla, nadharia teule imekuwa muafaka katika uchanganuzi wa data za makala hii.

## 4.0 UCHAMBUZI WA DATA NA MJADALA

Lengo la makala hii lilikuwa ni kuchunguza athari za ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu nchini Tanzania kwa wanajamii. Kama ilivyoelezwa awali katika kipengele cha 2.0 cha makala hii, data zilikusanywa kwa njia ya usaili na majadiliano katika makundi lengwa. Hivyo basi, watoataarifa walitakiwa kueleza matokeo ya maana zinazodokezwa katika majina ya wanajamii kwa watumiaji wa majina husika, ambazo ndizo data za utafiti huu. Aidha, watoataarifa 240 walishiriki katika utafiti huu na matokeo kuhusu athari za ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu kwa watumiaji wake yalikuwa kama ifuatavyo:

### 4.1 Ujinsia Hujenga na Kuimarisha Tabia za Wanajamii

Athari ya kwanza ya ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu kwa wanajamii ni kujenga na kuimarisha tabia za watumiaji wake. Kwa hiyo, data hizo zimeonesha kuwa jina la mtu si neno la utambulisho pekee, bali ni unabii, historia, na kioo cha tabia ya mtumiaji wa jina husika. Matokeo haya yanaashiria kwamba ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu una dhima ya kuumba, kuongoza, na kudhibiti mienendo na tabia za wanajamii. Mathalani, watoataarifa wanasema:

**Mtoataarifa Na. 1:**

*...jina linaumba na jina ni tabia...kile unachomwita mtoto ndicho kinachojitokeza katika tabia, mwenendo, au hatma ya maisha yake. Ukimuita mtu jina la baraka, anakuwa wa baraka; ukimuita mtu jina la fujo anakuwa wa fujo... kwa mfano mtu anayeitwa 'Mpole' akionekana kuwa mtulivu na mwenye heshima, watu watasema, ''kweli jina ni tabia'' au ''kweli jina huumba...*

**Mtoataarifa Na. 2:**

*...mtoto anapopewa jina la babu yake aliyekuwa kiongozi jasiri, mtoto huyo atarithi ujasiri na busara ileile. ...mara nyingi jina la mtoto hufundishwa tangu mdogo kwamba yeye ni mtu fulani, na fulani hakuwa muoga. Hii inamjenga kifikra kuwa jasiri...*

**Mtoataarifa Na. 3:**

*...mtoto anapokua na kujua maana ya jina lake, kama lina maana chanya, hujijengea hali ya kujiamini na kuishi kwa kufuata misingi ya jina hilo lakini jina baya linazalisha tabia mbaya.*

Data hizo zinaonesha kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ni nyenzo ya kiutamaduni inayotumika kuumba na kuimarisha tabia za wanajamii wa jamiilugha Kibantu. Kwa mfano, mtoataarifa namba 1 anaeleza kuwa jina la mtu huumba tabia na hatma ya mtu. Aidha, anasisitiza kuwa watoto wapewe majina yenye maana nzuri ili kuwajengea hatma nzuri. Vilevile, mtoataarifa namba 2 anaeleza kuwa jina la mtu humjenga na kumuimarisha mhusika kitabia tangu akiwa mdogo. Hivyo basi, jina la mtu ni muongozo wa fikra, imani na matendo yake. Kadhalika, mtoataarifa namba 3 anaeleza kuwa watu huishi katika mipaka ya majina yao. Yaani, mtu anapokua na kutambua maana na mazingira ya uteuzi wa jina lake, huishi kutokana na jina husika. Hata hivyo, mtoataarifa namba 3 anatoa msisitizo wa kwamba jina hujenga na kuimarisha tabia za mtu ikiwa na ikiwa tu mhusika atajua maana na mazingira ya uteuzi wa jina lake. Kwa mantiki hiyo, kwa kuwa imeripotiwa kuwa majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu hudokeza ujinsia unaowapendelea zaidi watoto wa kiume kuliko watoto wa kike (Buberwa, 2018a&b), basi ujinsia unaodokezwa katika majina hayo hujenga na kuimarisha tabia zinazojenga hadhi kubwa kwa watoto wa kiume kuliko watoto wa kike. Ni katika muktadha huo, tabia ya kujiamini, ujasiri, kuwa na msimamo, kufanya kazi kwa bidii, kuwa na tajriba ya shari, kutaka heshima, kutaka makuu, uadilifu, ushindani, na kuthubutu mambo makubwa hujengwa na kuimarishwa kwa watoto wa kiume. Aidha, tabia kama kupenda amani, furaha, unyenyekevu, upole, utii, kuhitaji kupendwa, kuhitaji kuhudumiwa, kuhitaji kusaidiwa, kupenda urembo, na kudeka ni tabia zinazojengwa na kuimarishwa kwa watoto wa kike wa jamiilugha za Kibantu nchini Tanzania. Hivyo basi, mila na desturi za Kibantu zimegawa tabia za wanaume na wanawake kijinsia. Kwa mantiki hiyo, jamii zingetaka watoto (wote wa kiume na wa kike) wawe na tabia zinazofanana ingewezekana. Vilevile, jamii zingehitaji tabia zilizohifadhiwa kwa wanaume ziwe za wanawake na zile za wanawake ziende kwa wanaume ingekuwa hivyohivyo kadri ya matarajio ya jamii. Kwa hiyo, tabia za wanajamii zimekitwa katika mila na desturi za jamii husika na hujengwa na kuimarishwa na vipengele mabimbali vya kiutamaduni, pamoja na ujinsia unaodokezwa katika majina ya watoto.

Aidha, Dong (2014) aneleza kuwa baada ya mtoto kuzaliwa, jamii hufanya mambo tofautitofauti kwa watoto wa kiume na wa kike ambapo mtoto wa kiume hupatiwa jina mahsusi lenye matarajio ya kurithisha muonekano, na majukumu ya kijamii. Kadhalika, Dong anaeleza kuwa jamii humtarajia mtoto wa kiume kuwa mtu mahiri, mwenye kujitegemea, jasiri, mwenye msimamo, na mwenye mtazamo chanya katika jamii. Hivyo basi, wanajamii hawateui majina kiholela tu, bali watoto hupatiwa majina mahsusi yaliyobeba matarajio ya tabia na majukumu yanayoendana na jinsia zao. Vilevile, matokeo ya utafiti huu yameegemea katika msingi wa Nadharia ya Ubabedume ya Bly (1970) unaodai kuwa maeneo ya ubabedume hujitokeza katika

desturi kwa ujumla kupitia maumbile, nguvu za kimwili, ushujaa, kufanya kazi, kukidhi mahitaji ya familia, kuwa na tajriba ya shari kijinsia, ukakamavu, urazini, kutaka makuu, majivuno, uadilifu, ushindani, na kuthubutu mambo makubwa. Msingi huo wa nadharia unadokeza baadhi ya tabia zilizohifadhiwa kwa ajili ya mtoto wa kiume wa Kibantu na humjengea heshima kubwa kuliko mtoto wa kike. Ni katika mazingira hayo ujinsia unaodokezwa katika majina ya wanaume hujenga na kuimarisha tabia za wanaume za utawala, uongozi, na umiliki wa rasilimali za jamii huku wanawake wakiwajengewa tabia za upole, unyenyekevu, utii, kufariji, na malezi zinazowafanya kuwa wasaidizi wa wanaume. Hata hivyo, kuna wanajamii ambao tabia zao haziendani na matarajio yaliyobebwa katika majina yao. Hali hiyo inaweza kuwa imechochewa na sababu mbalimbali ambazo ni pamoja na ukweli kuwa tabia za wanajmaii hujengwa na vipengele vingi vya kijamii na kiutamaduni, si ujinsia unaodokezwa katika majina yao pekee. Pia, baadhi ya wanajamii wanatumia majina zaidi ya moja. Kwa hiyo, ni vigumu kuthibitisha kuwa ni ujinsia unaodokezwa katika jina lipi kati ya majina waliyonayo umejenga na kuimarisha tabia zao. Hapa, kuna haja ya kufanyika utafiti wa kina utakaoweka wazi athari za ujinsia unaodokezwa katika majina ya wanajamii wanaotumia majina mengi. Sababu nyingine inayofanya baadhi ya watu wasiendane na ujinsia unaodokezwa katika majina yao ni kutokufahamu maana na mazingira yaliyoukilia uteuzi wa majina yao (Buberwa, 2018b). Ni katika mazingira hayo, inawezekana kabisa mtoto huathiriwa na jana lake ikiwa na ikiwa tu anafahamu maana na mazingira ya uteuzi wa jina hilo. Kwa hiyo, ikiwa mtu hafahamu maana na mazingira ya uteuzi wa jina lake, hukosa mshikamano na jina hilo kiasi cha kutokuendana nalo kabisa. Kwa ujumla, kwa sababu majina ya watu huathiri watumiaji wake kijinsia, watu wanapaswa kuteua majina kutoka katika lugha wanazozifahamu ili wahusika waweze kujua maana na mazingira ya uteuzi wake. Vilevile, mamlaka za uteuzi wa majina zinapaswa kuteua majina yanayobeba maana nzuri zinazojenga usawa kwa wanajamii (wote wanaume na wanawake).

**4.2 Ujinsia Huukilia Mamlaka za Watu katika Familia na Jamii**

Athari nyingine ya ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu kwa watumiaji wake ni kuukilia mamlaka za watu katika familia na jamii kwa ujumla. Kwa hiyo, ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ni nyenzo inayoamua mamlaka, nguvu, na hadhi za watu katika familia na jamii. Kwa mfano, watoataarifa wanasema:

**Mtoataarifa Na. 4:**

*...jina la mtu ni msingi wa kwanza wa mamlaka yake. Ukitaka kumtawala mtu, anza kwa kulijua au kulibadili jina lake...kijadi watawala wetu walikuwa wakipewa majina mapya ya kifalme ili kuwapa nguvu na uhalali wa kisheria na kisaikolojia juu ya watawaliwa...*

**Mtoataarifa Na. 5:**

*...kiasili mwenye jina linalohusu ukoo wa kiongozi, shujaa, au mtemi, anakuwa na mamlaka ya asili ya kusikilizwa kikaoni kuliko mtu mwenye jina la kawaida au la kifedhuli... jina lenye heshima linamlinda mtu na linampatia uwezo wa kuamuru na kunyoosha mambo... mwenye jina kama Mwamba, Mtemi, au Simba amebeba matarajio ya kuwa na sauti ya mamlaka tangu utotoni...*

**Mtoataarifa Na. 6:**

*...mtoto akipewa jina la mamlaka, jamii inamheshimu na kuwekeza kwake matarajio ya juu. Malezi hayo yanamfanya akue akiamini kuwa yeye ana jukumu la kuongoza. Jambo hilo linamjengea uwezo wa kujiamini na sauti ya mamlaka anapokuwa mtu mzima...*

Data hizo zinaonesha kuwa majina ya watu ni nyenzo ya ujenzi wa mamlaka za wanajamii katika ngazi ya familia na jamii kwa ujumla. Mathalani, mtoataarifa namba 4 anaeleza kuwa jina la mtu ni msingi wa kwanza wa mamlaka yake. Mwanajamii huyo anaendelea kwa kusema kuwa majina ya watu ni nyenzo ya utawala ambapo watawala hulazimika kufahamu majina ya watawaliwa ili kuweza kuwatawala sawasawa. Aidha, wakati mwingine viongozi hubadili majina yao ili kurahisisha tawala zao. Pia, wakati mwingine watawaliwa hubadilishiwa majina yao ya awali ili wasilete misukosuko wakati watawala wanatekeleza majukumu yao ya kiutawala. Kwa muktadha huo, jamii zinapaswa kuweka uzito na umakini mkubwa katika mchakato wa uteuzi wa majina ya watoto kama mkakati muhimu wa ukombozi kifikra, kiuchumi na kisiasa. Kadhalika, mtoataarifa namba 5 anaeleza kuwa historia za majina na maana zinazobebwa katika majina husika huukilia hadhi na nafasi za watu katika familia na jamii. Data hiyo inaonesha kuwa jina lenye heshima humlinda na kumpatia mtu uwezo wa kutekeleza majukumu yake kiutawala ilhali jina la kawaida au lenye maana mbaya hushusha hadhi na mamlaka za mtu katika familia na jamii. Vilevile, mtoataarifa namba 6 anaeleza kuwa jamii huwekeza matarajio makubwa yenye hadhi ya juu kwa watoto wenye majina yenye heshima na mamlaka kubwa. Wanajamii huwalea na kuwatendea wahusika sawasawa na maana zilizohifadhiwa ndani ya majina yao. Kwa kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu umekaa kitabaka ambapo majina ya wanaume hubeba maana nzuri zenye hadhi kubwa kuliko wanawake (Salihu, 2014, na Pilcher, 2017), basi ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu hujenga na kuendeleza mamlaka za wanaume katika familia na jamii huku wanawake wakijengwa kuwa wasaidizi tu. Kwa mantiki hiyo, mila, desturi, falsafa, na itikadi za jadi za jamiilugha za Kibantu humuandaa mtoto wa kiume kuwa na mamlaka makubwa ya kiuongozi na kumiliki rasilimali za familia na jamii huku wanawake wakiandaliwa kuwa wasaidizi wao.

Vilevile, matokeo hayo yamejengwa katika mhimili wa Nadharia ya Ubabedume ya Bly (1970) unaodai kuwa wanaume wametawala na kuwa na mamlaka makuu katika jamii kwa kushikilia nafasi na rasilimali zenye thamani katika jamii kama vile kazi, pesa, na taasisi za kijamii zenye nguvu kama serikali na dini. Mhimili huu wa nadharia unaashiria kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu huukilia utawala na mamlaka za wahusika katika familia na jamii kwa ujumla. Kwa muktadha huo, imeonekana kuwa mila na desturi za jamiilugha za Kibantu zimewapatia wanaume utawala na mamlaka makuu kuliko wanawake. Ingawa kwa sasa baadhi ya wanawake wameshikilia fursa na nafasi zenye heshima kubwa katika jamii kama vile uongozi katika taasisi za serikali na mashirika binafsi, idadi yao bado ni ndogo ikilinganishwa na wanaume. Vilevile, wanajamii wengi (wote wanaume na wanawake) bado wanaamini kuwa uongozi wa familia na jamii umehifadiwa kwa ajili ya mtoto wa kiume. Ni katika mazingira hayo jamii huwekeza matarajio makubwa ya kiutawala katika majina ya watoto wa kiume kuliko watoto wa kike. Kwa hiyo, ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu huwajenga watoto wa kiume kuwa watawala wa familia na jamii huku watoto wa kike wakijengwa kuwa wasaidizi tu. Kwa ujumla, wanajamii wanapaswa kuepuka mila na desturi zinazojenga na kuendeleza ubaguzi wa kijinsia katika familia na jamii. Mkakati mmojawapo unaojenga na kuendeleza usawa wa kijinsia ni kuteua majina yanayowapatia watoto (wote wa kiume na wa kike) mamlaka sawa katika familia na jamii kwa ujumla.

### 4.3 Ujinsia Husababisha Matatizo ya Kisaikolojia kwa Wanajamii

Baada ya kuchunguza maoni ya wanajamii kuhusua matokeo ya maana zilizobebwa katika majina ya watu imebainika kuwa ujinsia unaodokezwa katika baadhi ya majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu husababisha matatizo ya kisaikolojia kwa watumiaji wake. Kwa muktadha huo, imeonekana kuwa baadhi ya vipengele vya ujinsia vinavyodokezwa katika majina ya watu ni mizigo ya kisaikolojia vinavyomfanya mtu ajihisi mnyonge, mwenye hatia, au kutengwa katika familia na jamii yake. Mathalani, watoataarifa wanasema:

**Mtoataarifa Na. 7:**

*...kila niliposikia mwalimu akiita jina langu 'Tabu' darasani, sikuwa nasikia jina tu; nilikuwa nasikia tangazo la umaskini wetu. Lilininyonga mbele ya wanafunzi wenzangu... majina mabaya ni makovu ambayo hayaumi kwa kuguswa, yanauma kwa kutajwa na kuwaza akilini mwako...*

**Mtoataarifa Na. 8:**

*...majina yanayohusishwa na ukoo mbaya, uchawi, au mikosi inamsababishia mtu kuogopwa au kutengwa na jamii... ukiwa na jina la usumbufu unaweza kuanza kuwa msumbufu kweli kwa sababu akili yako imekaririshwa kuwa ndio unatakiwa kuwa hivyo. Jamani jina baya linasababisha msongo mkubwa wa mawazo...*

Data hizo zinaonesha nguvu zilizomo ndani ya majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu. Hata hivyo, badala ya jina kuwa utambulisho mwema kwa watu, baadhi ya majina huwa mizigo inayowaelemea wahusika kwa sababu huwakwaza na kuwasuta kwa hali walizonazo au walizowahi kuzipitia katika maisha yao. Kwa mfano, mtoataarifa namba 7 anaeleza kuwa jina lake si utambulisho pekee, bali ni mwangwi unaomkumbusha hali ya umaskini wa familia yao. Hivyo basi, jina lake ni chanzo cha huzuni na mahangaiko ya kisaikolojia. Vilevile, mtoataarifa namba 8 anaeleza kuwa majina yenye maana mbaya huleta madhara kwa watumiaji wake. Aidha, jina baya humshurutisha mhusika ili afanane nalo. Kwa mantiki hiyo, wanajamii wanapaswa kuepuka kuteua majina yenye maana mbaya kihistoria, na kiutamaduni. Pia, kwa kuwa majina mengi ya wanaume hudokeza ujinsia unaobeba maana nzuri na hadhi kubwa kuliko majina ya wanawake (Pondelíková na Štulajterová, 2024), basi wanawake wengi hupata matatizo ya kisaikolojia yanayochochewa na ujinsia unaodokezwa katika majina yao.

Vilevile, Wanyama (2022) alipochunguza mikakati ya uyahe na raghba ya ujinsia kama mkakati wa propaganda katika mdahalo wa uraisi wa Kenya, 2013 alibaini kuwa uyahe na raghba ya ujinsia hutumika kujenga sifa njema za wanaume huku ikilenga kubomoa sifa za wanawake. Matokeo ya utafiti wa Wanyama yanaashiria kuwa mila na desturi za Kiafrika bado zinalenga kuistawisha jinsia ya kiume huku zikibomoa ustawi wa jinsia ya kike. Vilevile, matokeo hayo yamekitwa katika mhimili wa Nadharia ya Ubabedume ya Bly (1970) unaodai kuwa utawala wa wanaume umehalalishwa katika kila sehemu ya maisha kwa kusisitiza maumbo ya vitambulishi vya jinsia ya kiume kwa misingi ya jamii, maandishi, na matukio au maelezo ya kihistoria. Kwa ujumla, imeonekana kuwa wanajamii wengi wa jamiilugha za Kibantu wanaopata madhara ya kisaikolojia kutokana na ujinsia unaodokezwa katika majina yao ni wanawake kuliko wanaume. Hali hiyo inatokana na kwamba utamaduni wa Kibantu umejengwa katika misingi ya mfumodume inayowapendelea zaidi watoto wa kiume kuliko watoto wa kike. Hivyo basi, wanajamii wanapaswa kuachana na baadhi ya mila na desturi za jadi zinazochochea ubaguzi wa kijinsia unaolenga kujenga hadhi nzuri kwa watoto wa kiume huku ukibomoa hadhi za watoto wa kike. Kutokana na mabadiliko na changamoto za kimaisha, kwa sasa watoto (wote wa kike na wa kiume) wanapaswa kushiriki kwa usawa katika shughuli za kimaendeleo katika familia na jamii. Kwa mantiki hiyo, ili waweze kushiriki kikamilifu kwa usawa, wote wanapaswa kuwa na hali nzuri ya kisaikolojia itakayowafanya kujiamini, wenye ubunifu, uhuru wa kijamii na kiutamaduni.

**4.4 Ujinsia Huukilia Mahusiano ya Wanajamii kwa Mungu na Wahenga**

Vilevile, utafiti huu ulibaini kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu huukilia mahusiano ya wanajamii kwa Mungu na wahenga. Hivyo basi, majina ya watu si tu ni alama ya utambulisho bali ni kiunganishi cha kiimani cha wanajamii na nguvu za asili na Mungu. Aidha, jina la mtu ni madhabahu ya kiroho, alama ya shukurani, na agano la wanajamii na Mungu au wahenga. Kwa mfano, watoataarifa wanasema:

**Mtoataarifa Na. 9*:***

*...jina linamuunganisha mtoto na wakubwa waliotangulia. Majina yetu yanaonesha kwamba mizimu haijatutupa, bali inatembea nasi katika damu mpya...*

**Mtoataarifa Na. 10:**

*...jina langu si utambulisho wangu kwa wanadamu tu; ni sala fupi inayorindima kila ninapoitwa, linamkumbusha kila mtu kuhusu ukuu na wema wa Mungu katika maisha yangu...*

**Mtoataarifa Na. 11:**

*...hata katika Biblia Takatifu imeelezwa pale Mwanzo 17:5 kwamba, ''wala jina lako lisiitwe tena Abramu, lakini jina lako litakuwa Ibrahimu; kwani nimekufanya kuwa baba wa mataifa mengi''. Lazima mtu uwe na jina linalompa heshima na utukufu Mungu...*

Data hizo zinaonesha kuwa baadhi ya vipengele vya ujinsia vinavyodokezwa katika majina ya watu huukilia mahusiano ya wanajamii kwa Mungu na wahenga wao. Kwa hiyo, baadhi ya majina ya watu huwaweka watu karibu zaidi na wahenga na Mungu wao kuliko majina mengine. Kwa mfano, mtoataarifa namba 9 anaeleza kuwa, kiimani, jina la mtoto ni kipengele kimojawapo cha ibada kinachomuunganisha mtu kiroho na wahenga wake. Vilevile, mtoataarifa namba 10 anaeleza kuwa baadhi ya majina ni sala fupi inayowakumbusha wanajamii kuhusu ukuu na wema wa Mungu katika maisha yao. Kadhalika, mtoataarifa namba 11 anasisitiza kuwa lazima wanajamii wateue majina yanayompatia Mungu heshima na utukufu. Kwa mantiki hiyo, data za utafiti huu zimeonesha kuwa jina la mtu ni nyenzo muhimu ya kiimani. Aidha, kwa kutumia nukuu iliyotolewa katika biblia takatifu na mtoataarifa namba 11, inaashiria kuwa baadhi ya majina yanakubalika zaidi kiimani kuliko mengine. Kwa hiyo, nukuu inaonesha maagizo ya Mungu ya mabadiliko ya jina kutoka kuitwa '*Abramu*' kwenda '*Ibrahimu*' ili kutengeneza ukaribu mzuri wa mhusika na Mungu wake. Aidha, mahitaji ya watu kutaka kuwa karibu ba Mungu na wahenga ni sababu mojawapo inayochochea dini mbalimbali kuwapatia waamini wake majina mapya yanayokubalika zaidi katika imani ya dini husika.

Vilevile, uzoefu wa mtafiti unaonesha kuwa, katika imani za jadi za Kiafrika, baadhi ya watoto hubadilishiwa majina yao kama njia ya kutekeleza maagizo ya kiroho ya wahenga. Wanajamii wasipotekeleza maagizo hayo hutokea matatizo makubwa kwa watoto au jamii kwa ujumla. Haya yote yanaonesha kuwa majina ya watu yana nguvu kubwa kiimani. Hata hivyo, kutokana na majina ya watu yanayoonesha uhusiano wa wahusika kwa Mungu na wahenga huwapendelea zaidi wanaume kwa kuwaweka karibu zaidi kwa Mungu na wahenga kuliko wanawake (Salihu, 2014; Buberwa, 2018a na Wappa na Wada, 2019), basi ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu huwaweka wanaume karibu zaidi kwa Mungu na wahenga kuliko wanawake. Kwa mantiki hiyo, mila na desturi za jamiilugha za Kibantu huwajenga na kuwaendeleza wanaume kuwa na mamlaka makubwa kiimani inayowafanya kuwa viongozi na wamiliki wa rasilimali za familia na jamii huku wanawake wakibaki kuwa wasaidizi tu. Vilevile, matokeo hayo yamejengwa katika mhimili wa Nadharia ya Ubabedume ya Bly (1970) unaodai kuwa wanaume wameweka utambulisho wao katika sura na mfano wa Mungu kwa manufaa yao wakizingatia kwamba mwanaume alipewa mwanamke kama mwenzi kutoka kwa Mungu ambaye ni wa kiume. Mhimili huo wa nadharia unaashiria kuwa hali ya ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu kuwapendelea zaidi wanaume kwa kuwaweka karibu zaidi kwa Mungu na wahenga imechochewa na mila, desturi, na matarajio ya wanajamii yaliyojengwa katika misingi ya mfumodume inayowapatia wanaume uongozi na mamlaka makubwa kuliko wanawake. Ni katika mazingira hayo mila na desturi za Kiafrika zimempatia mwanaume kipaumbele katika majukumu mazito na muhimu katika jamii, pamoja na jukumu la uteuzi wa majina kwa watoto wao kama njia mojawapo ya kutoa baraka na unabii kuhusu hatma za watoto na jamii kwa ujumla (Mensah, 2023). Kwa ujumla, ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu humjenga na kumuendeleza mtoto wa kiume kuwa karibu zaidi kwa Mungu na wahenga kuliko mtoto wa kike. Matokeo hayo ya utafiti yanaonesha umuhimu wa wanajamii kuweka usawa kwa watoto (wote wa kiume na wa kike) kwa kuwaweka karibu na Mungu na wahenga kupitia mila na desturi zao, pamoja na kuteua majina jumuishi yasiyodokeza ubaguzi wa kijinsia.

**4.5 Ujinsia Huukilia Mgawanyo wa Majukumu Kiutamaduni kwa Wanajamii**

Athari nyingine ya ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu ni kuukilia mgawanyo wa majukumu kiutamaduni kwa wanajamii. Kwa mantiki hiyo, jina la mtu si utambulisho wa sura unaomtofautisha mtu mmoja na mwingine pekee (Bichwa, 2025), bali ni mkataba wa kijamii unaoukilia mienendo na majukumu ya wanajamii kiutamaduni. Aidha, majina ya watu hubeba matarajio, kazi, na nafasi ambayo mhusika anapaswa kuijaza katika familia na jamii yake. Mathalani, watoataarifa wanasema:

**Mtoataarifa Na. 12:**

*...unapompa mtoto jina, unampa muongozo wa majukumu yake katika ukoo. Jina la mtu ndilo huamua kama atakuwa mlinzi wa boma au mlimaji wa mashamba au mfugaji... majina mengine ni amri ya kijadi tangu utotoni. Yanapofika masikioni kwa mtoto, hayamwambii tu kwamba 'wewe ni nani', yanamwambia 'unapaswa kufanya hili, fanya lile, hupaswi kufanya hili...*

**Mtoataarifa Na. 13:**

*...kila nikiitwa jina langu, siitwi mimi tu kama binti; ninakumbushwa jukumu langu la kulinda wadogo zangu na kusimamia boma. Jina langu ni kazi yangu ya kila siku na ninajitahidi kuendana nalo kwa sababu linanipa nguvu ya kuwa jinsi nilivyo...*

Data hizo zinaonesha kuwa baadhi ya vipengele vya ujinsia vinavyodokezwa katika majina ya watu huukilia mgawanyo wa majukumu kiutamaduni kwa wanajamii. Kwa mantiki hiyo, majina ya watu huchangia kwa wanajamii kufanya au kutokufanya shughuli fulani. Kwa mfano, mtoataarifa namba 12 anaeleza kuwa majina ya watu ni miongozo ya majukumu wanayopaswa kutekeleza katika familia, ukoo, na jamii kwa ujumla. Aidha, imeelezwa kuwa baadhi ya majina ya watu hutoa amri za kijadi kwa wanajamii kuhusu majukumu yao kiutamaduni tangu utotoni. Vilevile, mtoataarifa namba 13 anaeleza kuwa majina ni mwangwi unaowakumbusha wanajamii kuhusu majukumu yao ya kila siku. Pia, imeonekana kuwa majina ya watu huwafinyanga na kuwajenga wahusika ili kuendana na matarajio yaliyobebwa ndani yake. Ni katika mazingira hayo wanajamii wakisikia jina la mtu, hata kama hawajamuona mhusika, watafahamu jinsia na majukumu yanayopaswa kutekelezwa naye. Hvyo basi, data za utafiti huu zinaonesha kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu huukilia mgawanyo wa majukumu ya wanajamii. Kwa hiyo, kwa kuwa majukumu ya kiutamaduni ya wanajamii wa jamiilugha za Kibantu yamekitwa katika misingi ya mfumodume inayowapendelea zaidi watoto wa kiume (Nyangaywa, 2013; na Lusekelo na Mtenga, 2020), basi ujinsia unaodokezwa katika majina hayo huukilia mgawanyo wa majukumu kiutamaduni yanayompatia mtoto wa kiume heshima na mamlaka makubwa zaidi kijamii na kiutamaduni kuliko mtoto wa kike.

Aidha, AbdAlgane (2021) anaeleza kuwa uteuzi wa msamiati unaofanywa na wazungumzaji na waandishi una athari kwa wasikilizaji au wasomaji na huzalisha na kuendeleza upendeleo wa kijinsia au dhana za awali zilizoamiliwa hata kama wapokeaji wa ujumbe hawana mwelekeo wa ujinsia. Matokeo hayo yanaashiria kuwa majina ya watu huwaathiri watumiaji wake kijinsia hata kama wahusika hawana mwelekeo wa kijinsia. Ni katika mazingira hayo, imebainika kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya Kibantu huukilia majukumu kiutamaduni ya wanajamii kijinsia hata kama wanajamii hao hawana mwelekeo wa ubaguzi wa kijinsia. Hivyo basi, wanajamii hujengwa na huandaliwa kutekeleza majukumu yao kijinsia kupitia majina wanayopatiwa utotoni. Vilevile, matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na mhimili wa Nadharia ya Ubabedume ya Bly ya (1970) unaodai kuwa maeneo ya ubabedume hujitokeza katika desturi kwa ujumla kupitia maumbile, nguvu za kimwili, ushujaa, kufanya kazi, kukidhi mahitaji ya familia, kuwa na tajriba ya shari ya kijinsia, ukakamavu, urazini, kutaka makuu, majivuno, uadilifu, ushindani, na kuthubutu mambo. Mhimili huu wa nadharia unaonesha msingi wa mgawanyo wa majukumu kiutamaduni unaowajenga na kuwaendeleza wanaume kuwa viongozi, watawala, na wamiliki wa rasilimali katika familia na jamii huku wanawake wakiachiwa nafasi ya kutekeleza majukumu yote katika familia kama vile, kupika, usafi, malezi, kuhifadhi chakula, na kuwafariji wanafamilia.

Hivyo basi, ni katika mazingira hayo wanajamii wengi wa jamiilugha za Kibantu huamini kuwa mwanaume ndiye kichwa cha familia kutokana na majukumu yake kiutamaduni huku mwanamke akipatiwa jukumu la usaidizi kiutamaduni. Hata hivyo, kwa sasa, majukumu na shughuli za uzalishaji mali zimeanza kuondoka katika misingi ya mfumodume inayowapendelea zaidi wanaume. Kwa mfano, uzoefu unaonesha kuwa, katika baadhi ya familia, watoto wa kike na wa kiume hushirikiana katika shughuli za nyumbani kama vile kufua nguo, kupika, kuosha vyombo, kuteka maji, kuchanja kuni, na usafi wa nyumba. Vilevile, wanaume na wanawake wanashiriki katika shughuli za kiuchumi na kiuongozi bila kuwekewa mipaka kijinsia. Hali hii inaashiria kuwa jamiilugha za Kibantu zimeanza kupokea mabadiliko na changamoto zinazochochea jamii kuanza kuachana na baadhi ya mila na desturi zinazogawanya majukumu kijinsia. Hata hivyo, ingawa jamii zimeanza kupokea mabadiliko ya mila na desturi yanayoonesha matumaini ya wanajamii kuishi katika usawa bila kubaguana kijinsia, wanajamii wengi wa Kibantu bado wanaamini katika mila na desturi zinazogawanya majukumu ya wanajamii kijinsia. Ni katika muktdha huo imeonekana kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu wa jamiilugha za Kibantu nchini Tanzania huzalisha na kuendeleza mgawanyo wa majukumu kiutamaduni kwa wanajamii ambapo wanaume hutoka na kwenda kujumuika katika jamii kwa ajili ya kutafuta mahitaji ya familia huku wanawake wakibaki nyumbani kwa ajili ya kutekeleza shughuli zote za nyumbani. Mgawanyo huo wa majukumu kijinsia hujengwa na kuendelezwa kupitia vipengele vya mila na desturi, pamoja na mchakato wa uteuzi wa majina ya watoto.

**4.6 Ujinsia Huukilia Mafanikio ya Wanajamii**

Data zilizokusanywa kwa njia ya usaili na majadiliano katika makundi lengwa zimebainisha kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu huukilia mafanikio ya wanajamii wanaotumia majina husika. Mathalani, watoataarifa wanasema:

**Mtoataarifa Na. 14:**

*...kama wasanii wanakuwa na majina fulani hivi yanayo-push kazi zao. Ukiwa na jina ambalo halielewekieleweki utayasikia tu mafanikio... jina linamsaidia sana mtu katika maisha yake. Jina baya linavuta nuksi na mabalaa lakini jina zuri linafungua milango ya baraka na mafanikio... hata kwenye kutafuta mwenza tunaangalia na jina lake bwana...*

**Mtoataarifa Na. 15:**

*...tusiwachurie watoto wetu kwa kuwapa majina ya ajabuajabu kisa eti sijui la babu yake, la nani yake. Kila mtu ana maisha yake, hao wenye majina hawakuacha mali za kurithi, ndio warithishe majina? Siwezi kumchuria bure mwanangu, kisa nini? Tena mtoto wa kike na dunia hii ya leo ndio umpe jina la mitishamba na uganga? Hapana, majina yanaumba jamani tusiwaharibie watoto wetu. Kuna majina mazuri tu hata kwenye tamthilia tunaziona...*

Data hizo zinaonesha kuwa majina ya watu yana mchango katika mafanikio na maendeleo ya watu katika jamii. Kwa mfano, mtoataarifa namba 14 anaeleza kuwa, katika harakati za utafutaji mali na maendeleo, baadhi ya watu hufanya mabadiliko mbalimbali katika maisha yao, pamoja na kubadili au kuongeza majina yanayowawezesha kutimiza ndoto zao. Aidha, mwanajamii huyo anasisitiza kuwa majina yenye maana mbaya hufungua milango ya kuingiza mabalaa, mikosi, matatizo, na umaskini kwa watumiaji wake. Kwa upande mwingine, majina yenye maana nzuri hufungua milango ya bahati, neema na baraka zinazowapeleka wanajamii kwenye mafanikio mazuri. Mtoataarifa huyo anakwenda mbele zaidi kwa kueleza kuwa jina la mtu linamchango katika kupata mwenza. Hali hii inaashiria kuwa mtu anaweza akakosa mambo muhimu, hata ajira, kwa sababu ya jina lake. Hali hii inaashiria kuwa baadhi ya vipengele vya mila na desturi ni hatari sana kwa wanajamii. Aidha, mtoataarifa namba 15 anatoa rai kuwa wazazi wateue majina yatakayowatabiria na kuwajengea watoto wao mambo mema.

Hata hivyo, mwanajamii huyo anaibua ukinzani katika maelezo yake pale anapoeleza kuwa wazazi wanaweza wakateua majina ya watoto wao kutoka kwenye vyanzo mbalimbali kama vile kutoka katika tamthiliya. Ukinzani uliopo hapa unatokana na kuwa kuna tamthiliya kutoka katika jamiilugha nyingi duniani; zipo tamthiliya za Kituruki, Kikorea, Kichina, Kihindi, Ki-Nigeria, kwa kutaja baadhi tu ambazo majina ya wahusika hutoka katika jamiilugha husika. Aidha, maana zinazobebwa katika majina ya wahusika wa tamthiliya hizo hazifahamiki kwa wanajamii wengi. Kwa hiyo, inaonekana kuwa baadhi ya wanajamii huteua majina kutoka katika kazi za sanaa kutokana na hali ya kuwapenda sana wahusika pasipokuchunguza maana na mazingira ya uteuzi wa majina hayo. Vilevile, sifa, tabia, na majina mengi ya wahusika wa kazi za sanaa si halisi na huteuliwa kwa madhumuni ya sanaa ili kuwasilisha ujumbe na uzuri wa kisanaa (Wamitila, 1999). Kwa hiyo, majina ya wahusika wa kazi za sanaa hayaendani na mazingira halisi ya kila mtu katika kila jamii. Wanajamii wanapaswa kuteua majina kutoka katika lugha na tamaduni zao. Kadhalika, mtoataarifa namba 15 anaeleza kuwa majina ya wanawake yanapaswa kutofautiana na majina ya wanaume, hii ni desturi inayozalisha na kuendeleza matabaka ya kijinsia katika jamii.

Aidha, kwa kuwa majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu yamebainika kuwa hudokeza ujinsia unaowapendelea zaidi wanaume kuliko wanawake (Buberwa, 2018a&b), basi ujinsia huo huwajenga na kuwapatia watoto wa kiume mafanikio makubwa zaidi kuliko watoto wa kike. Kwa mfano, mila na desturi za Kibantu huwajenga wanaume kuwa viongozi, watawala, wamiliki wa rasilimali, na wenye kukidhi mahitaji ya familia huku wanawake wakijengwa kufanya mambo madogomadogo ya kusaidia waume zao, malezi, na kutekeleza shughuli zote za nyumbani (Pilcher, 2017). Vilevile, matokeo yamejengwa katika msingi wa Nadharia ya Ubabedume ya Bly (1970) unaoeleza kuwa wanaume wametawala na kuwa na mamlaka makuu katika jamii kwa kushikilia nafasi za rasilimali zenye thamani katika jamii kama vile kazi, pesa, na taasisi za kijamii zenye nguvu kama serikali na dini. Msingi huo wa nadharia unaashiria kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu umejengwa katika misingi ya kiutamaduni, pamoja na desturi ya uteuzi wa majina ya watu inayoendeleza mfumodume ambao huwapatia wanaume mafanikio zaidi kuliko wanawake. Hivyo basi, ukombozi wa msingi wa maisha ya watu katika jamii ni pamoja na wanajamii kuteua majina kutoka katika jamiilugha zao yanayotabiri na kujenga hatma njema kwa watoto wao. Aidha, majina jumuishi yasiyodokeza ubaguzi wa kijinsia ni ufunguo wa mafanikio kijamii, kisiasa, na kiuchumi.

### 4.7 Ujinsia Hudhibiti Mawanda ya Upataji wa Maarifa kwa Wanajamii

Athari nyingine ya ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu ni kudhibiti mawanda ya upataji wa maarifa kwa wanajamii wanaotumia majina husika. Kwa hiyo, majina ya watu hutumika kama pasi ya kuingilia au kikwazo kinachoamua nani apate maarifa gani na kwa kiwango gani. Kwa mfano, watoataarifa wanasema:

**Mtoataarifa Na. 16:**

*...maarifa ya asili na uongozi wa kimila hutolewa kwa watu maalumu katika ukoo. Mara nyingi utamjua tu kwa jina lake kwa sababu majina yao yanakuwa ya wahenga waliotukuka. Mtoto anayepewa jina la 'Katemi' anafunguliwa milango ya chuo cha siri cha hekima ya jamii kuliko mwenye jina la kawaida tu...*

**Mtoataarifa Na. 17:**

*...ukizaliwa na kuitwa jina la ukoo wa wahunzi au waganga, unakuwa umetengenezewa hatma yako tangu utotoni. Jina linakuonesha kabisa kwamba huyu mtu anaweza zaidi upande gani wa maisha na*

*asipofuatilia anakuwa mtu wa kufanya hili hafanikiwi, anafanya lile hafanikiwi kwa sababu anakwepa sehemu yake...*

**Mtoataarifa Na. 18:**

*...majina ya unyonge yanaipa unyonge akili ya mtu. Yanafanya mtu aamini kuwa yeye hana uwezo wa kubeba maarifa mazito... wenye majina ya ushindi na mapambano au ushujaa wanakuwa na mafanikio kutokana na kwamba majina yao yanawasukuma kupata maarifa na kufanikiwa...*

Data hizo zinaonesha kuwa baadhi ya majina ya watu hudhibiti fursa za wanajamii kupata maarifa. Aidha, majina hutumika kama nyenzo ya kuchorea ramani na mipaka ya maarifa ya wanajamii. Mathalani, mtoataarifa namba 16 anaeleza kuwa watu wengi wenye maarifa mbalimbali katika jamii hutambulika kwa majina yao. Vilevile, mtoataarifa namba 17 anaeleza kuwa majina ya watu huweka mipaka ya aina na viwango vya maarifa wanayopaswa kupata. Kadhalika, mtoataarifa namba 18 anaeleza kuwa majina ya watu huwaathiri watumiaji wake kwani majina ya ushindi huwapatia ushindi watumiaji wake huku majina ya unyonge huwanyong'onyesha wanajamii kiakili. Kwa muktadha huo, imeonekana kuwa majina ya watu ni kipimo na ufunguo wa maarifa kwa wanajamii kwani majina yenye matarajio mazuri na makubwa huwajenga na kuwaendeleza wahusika kupata maarifa mengi na makubwa huku majina yaliyobeba matarajio ya kawaida huminya fusra na viwango vya upataji wa maarifa kwa wanajamii. Hata hivyo, Buberwa (2018a&b), Formato na Somma (2023), na Pondelíková na Štulajterová (2024) wameripoti kuwa majina yanayodokeza matarajio ya wazazi kwa watoto wao yamekaa kijinsia. Yaani, majina yenye matarajio mazuri na yenye hadhi kubwa hujitokeza zaidi kwa wanaume kuliko wanawake. Hivyo basi, kwa kuwa imebainika kuwa majina ya watu hudhibiti mawanda ya upataji wa maarifa kwa wanajamii, basi majina mengi ya wanaume huwapatia watumiaji wake mawanda makubwa zaidi ya upataji wa maarifa kuliko majina ya wanawake. Ni katika mazingira hayo imeonekana kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu huwajenga na kuwaendeleza wanaume kupata maarifa ya uongozi, utawala, udhibiti na uendelezaji wa rasilimali, utatuzi wa migogoro, mapambano, na ulinzi huku wanawake wakijengwa na kuendelezwa kuwa na maarifa ya malezi, na shughuli zote za nyumbani.

Kadhalika, matokeo hayo yamejengwa katika mhimili wa Nadharia ya Ubabedume ya Bly (1970) unaodai kuwa maeneo ya ubabedume hujitokeza katika desturi kwa ujumla kupitia maumbile, nguvu za kimwili, ushujaa, kufanya kazi, kukidhi mahitaji ya familia, kuwa na tajriba ya shari ya kijinsia, ukakamavu, urazini, kutaka makuu, majivuno, uadilifu, ushindani, na kuthubutu mambo. Mhimili huo wa nadharia unadokeza vipengele vya ubabe wa wanaume vinavyowapatia wahusika mawanda makubwa ya upataji wa maarifa. Kwa ujumla, mila, desturi, falsafa, na itikadi za jadi za Wabantu humjenga na kumuimarisha mtoto wa kiume kwa kumpatia mazingira rahisi ya upataji maarifa mengi yanayomjengea uwezo wa kufikia matarajio ya wazazi na wanawajamii, tofauti na wanawake ambao hujengewa mazingira ya kupata maarifa ya malezi na kutekeleza majukumu ya nyumbani pekee. Hata hivyo, uhusiano huu wa kiutamaduni umekuwa nguzo imara ya ustawi wa familia za Wabantu ambapo wanaume na wanawake hupata maarifa bora yanayowawezesha kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Ingawa kwa sasa kuna mivutano na mijadala mingi mikubwa inayochochewa na mabadiliko ya kimtazamo na kiutamaduni kuhusu usawa wa kijinsia, wanajamii wengi wanaona kuwa mabadiliko yanayopigania usawa wa kijinsia yanaenda kinyume na asili ya uumbaji na yanalenga kuchochea migogoro katika familia na jamii. Ni katika muktadha huo ndio maana imeonekana kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu bado unadhibiti mawanda ya upataji wa maarifa unaowapendelea zaidi watoto wa kiume kuliko watoto wa kike.

### 4.8 Ujinsia Huchochea Wanajamii Kuchukia Lugha na Tamaduni Zao

Athari ya mwisho ya ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu ni kuchochea wanajamii kuchukia lugha na tamaduni zao. Mathalani, watoataarifa wanasema:

**Mtoataarifa Na. 19:**

*...majina mengine yana maana mbaya kabisa. Unakuta mtu ana jina ambalo hata yeye mwenyewe hajisikii amani. Ndiyo maana unakuta mtu anaamua kubadilisha jina. Wengine wanatumia majina waliyopewa kwenye dini zao kwa sababu wanaepuka kutumia majina yao ya nyumbani...*

**Mtoataarifa Na. 20:**

*...hata kama ni utamaduni ndio umpe mtoto jina ambalo hata anaona aibu kuitwa? Tuwachagulie watoto majina mazuri. Mbona majina ya dini hayana shida? Kwa nini sisi tukomae na majina mabaya eti kisa utamaduni?...sawa utamaduni ni wetu lakini mbona wengine wana majina mazuri tu na wote ni wa hapahapa tu?*

Kwa mujibu wa data hizo, imeonekana kuwa baadhi ya wanajamii hujenga chuki kwa lugha na tamaduni zao kutokana na maana zinazodokezwa katika majina yao. Kwa mfano, mtoataarifa namba 19 anaeleza kuwa baadhi ya majina huwanyima amani wanajamii. Kutokana na hali hiyo, baadhi ya watu huchukua hatua za kubadilisha majina hayo na kuteua majina mengine kutoka katika dini na lugha za kigeni kama njia ya kuepuka athari za majina mabaya kama ilivyobainika vilevile katika Nyangaywa (2013), Madila (2020), Lusekelo na Mtenga (2020) na Buberwa (2022). Kadhalika, mtoataarifa namba 20 ameenda mbali zaidi kwa kusaili nafasi ya utamaduni katika uteuzi wa majina ya watu. Yeye, anaona kuwa watu wasiteue majina

mabaya kwa mgongo wa utamaduni. Yaani, utamaduni si kuteua majina yenye maana mbaya. Kwa ujumla, imebainika kuwa baadhi ya majina ya watu huchochea wahusika kuchukia lugha na tamaduni za jamiilugha husika. Kwa kuwa imeripotiwa kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu huwapendelea zaidi wanaume kwa kuwajengea hadhi nzuri ya utawala, uongozi, na kumiliki rasilimali za familia na jamii kuliko wanawake (Salihu, 2014; Pilcher, 2017; Buberwa, 2018a&b; na Mensah, 2023), basi ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu huwachochea wanawake wengi kuchukia lugha na tamaduni zao. Kutakana athari hiyo, ni wazi pia kwamba wanawake wengi wapo katika mazingira ya kubadilisha majina yao kama njia ya kuepuka athari za ujinsia unaodokezwa katika majina yao. Hapa, utafiti wa kina unahitajika ili kuweka wazi kiwango cha ubadilishaji wa majina ya wanawake na sababu zingine zinazoukilia wanawake kubadili zaidi majina yao. Aidha, hali ya wanawake wengi kuchukia lugha na tamaduni zao inatokana na ukweli kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu umejengwa katika mila na desturi zinazoendeleza mfumodume unaowapatia hadhi nzuri zaidi watoto wa kiume na kuwakadamiza watoto wa kike.

Hata hivyo, inapaswa kueleweka kuwa kuteua majina kutoka lugha za kigeni si suluhu ya migogoro ya kisaikolojia inayochochewa na baadhi ya majina ya watu kudokeza maana zinazodhaniwa kuwa ni mbaya. Hii ni kwa sababu uteuzi wa majina kutoka katika lugha za kigeni unakabiliwa na changamoto nyingi (Buberwa, 2022). Chngamoto hizo ni pamoja na baadhi ya majina ya kigeni kuwa magumu kutamkwa, baadhi ya majina hukosewa tahajia, baadhi ya majina hujitokeza katika maumbo mbalimbali, majina ya kigeni yakitumika hupoteza dhima yake ya utambulisho wa jamii, na majina ya lugha za kigeni huhifadhi na kuendeleza historia ya jamii za kigeni. Kwa ujumla, baadhi ya majina ya watu kutoka katika kila lugha hubeba maana mbaya huku mengine yakidokeza maana nzuri. Uwezo wa kutambua maana zinazodokezwa katika majina huchangiwa na viwango vya umahiri walivyonavyo wanajamii kuhusu lugha na utamaduni wake. Ikiwa wanajamii hawana umahiri wa lugha husika hawatafahamu uzuri au ubaya unaodokezwa katika majina yao. Hivyo basi, data za utafiti huu zinaashiria kuwa baadhi ya wanajamii huchukia majina kutoka katika lugha zao za asili kwa sababu wana umahiri wa kutambua maana zinazodokezwa katika majina husika, tofauti na majina ya kigeni ambayo hawafahamu maana zake (Buberwa, 2018b).

Aidha, mchakato wa uteuzi wa majina ya watu umekitwa katika misingi ya mila na desturi za jamiilugha husika, tabia au sifa za mtu, imani kwa wahenga na mizimu, maumbile, mwonekano, hali ya ujauzito, na masaibu mbalimbali (Baitan, 2010; Buberwa, 2018a&b; na Wappa na Wada, 2019). Kwa mantiki hiyo, baadhi ya majina ya watu yenye maana mbaya huteuliwa kwa makusudi ili kutunza historia na kukomesha matatizo na changamoto zilizowahi kutokea katika familia, ukoo, au jamii, yasije yakajirudia tena. Vilevile, mawazo ya kwamba uteuzi wa majina kutoka kwenye dini huepusha madhara yanayotokana na majina yanayodokeza ubaguzi wa kijinsia kama ilivyoelezwa na mtoataarifa namba 19, yanasailika. Kimsingi, inaonekana kuwa wanajamii huteua majina ya watoto wao kutoka kwenye dini zao na lugha za kigeni kwa sababu kuu mbili; kwanza, majina husika hurejelea watakatifu, watu mashuhuri, na watu waliodhaniwa kuwa waadilifu na wenye matendo mema. Kwa hiyo, wanajamii wengi huvutiwa na majina hayo kwa kudhani kuwa majina husika huwajenga na kuwafanya wafanane na wenye majina hayo. Pili, wanajamii huteua majina kutoka kwenye dini zao na lugha za kigeni kwa sababu hawajui maana na mazingira yaliyoukilia uteuzi wa majina husika. Mathalani, Buberwa (2018b) anaeleza kuwa 56.25% ya wanajamii hawafahamu maana zinazodokezwa katika majina yao, huku 61.25% ya wanajamii hawafahamu mazingira yaliyoukilia uteuzi wa majina wanayotumia. Aidha, Buberwa anaendelea kwa kusema kuwa sababu za wanajamii wengi kutokufahamu maana zinazodokezwa na majina yao, na kutokufahamu mazingira yaliyoukilia uteuzi wa majina hayo ni pamoja na matumizi ya majina kutoka kwenye dini zao, na majina mengine kutoka katika lugha za kigeni. Matokeo hayo yanaonesha kuwa, pengine, wanajamii wakifahamu maana zilizobebwa katika majina wanayoyapata katika dini zao, na mazingira yaliyoukilia uteuzi wa majina hayo watabadili mtazamo na kuchukua mwelekeo tofauti kabisa. Aidha, wanajamii watapata maarifa kuwa watakatifu na watu mashuhuri wanaotajwa kwenye dini za kigeni, walipewa majina kwa misingi ya tamaduni na mazingira yao. Vilevile, wanajamii watabaini kuwa kuna watu wengi wenye majina yaleyale lakini si watakatifu au watu mashuhuri kama walivyotarajiwa. Kwa hiyo, hakuna haja ya kupambania jina kutoka katika jamiilugha fulani kwa sababu za kutaka kufanana na mtumiaji wa jina husika. Pia, wanajamii wataachana na kasumba hiyo kwa sababu watapata maarifa kwamba uteuzi wa majina ya watu huukiliwa na mazingira tofautitofauti ya wahusika. Kwa mantiki hiyo, huwezi kutumia mazingira ya mtu mmoja kumpatia jina mtu mwingine. Suala linalokubalika kwa haraka bila mashaka makubwa sana ni kuwa majina ya watu yanapaswa kudokeza maana nzuri zinazofahamika kwa wanajamii ili, kama kuna athari zozote, yatoe athari nzuri kwa watumiaji wake.

Pia, matokeo ya utafiti huu yanakubaliana na msingi wa Nadharia ya Ubabedume ya Bly (1970) unaodai kuwa utawala wa wanaume umehalalishwa katika kila sehemu ya maisha kwa kusisitiza maumbo ya vitambulishi vya jinsia ya kiume kwa misingi ya jamii, maandishi, na matukio au maelezo ya kihistoria. Msingi huo wa nadharia unaashiria kuwa mwanaume huongoza na kutawala michakato mbalimbali ya kiutamaduni, pamoja na mchakato wa uteuzi wa majina ya watoto, ambayo hutumika kuzalisha, kuendeleza, na kuimarisha nafasi na taswira yake katika jamii. Kwa muktadha huo,

majina ya watoto wa kiume hulenga kujenga sifa bora za wanaume za uongozi na utawala zinazowafanya wahusika kuona fahari huku majina ya wanawake yakiwajengea wahusika nafasi ya usaidizi wa wanaume, unyenyekevu, utiifu, upole, ulezi, uoga, furaha, kupenda amani, na kutekeleza majukumu ya nyumbani. Ni katika muktadha huo, wanawake wengi hujenga chuki dhidi ya lugha na tamaduni zao kiasi cha kufikia kubadili au hurekebisha majina yao kama njia ya kujitibu majeraha ya kisaikolojia na kujinasua katika minyororo ya kiutamaduni yenye ubaguzi wa kijinsia. Ni katika mazingira hayo imeonekana kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu huchochea wanajamii kuchukia lugha na tamaduni zao.

## 5.0 HITIMISHO

Makala hii imechunguza kipengele cha uteuzi wa majina ya watu kwa lengo la kufafanua athari za ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu nchini Tanzania kwa watumiaji wa majina husika. Matokeo ya data zilizokusanywa zinaonesha kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu huwaathiri watumiaji wa majina husika kwa namna tofautitofauti. Athari hizo ni pamoja na kwamba ujinsia hujenga na kuimarisha tabia wanajamii, huukilia mamlaka za watu katika familia na jamii, na husababisha matatizo ya kisaikolojia kwa wanajamii. Vilevile, ujinsia huukilia mahusiano ya wanajamii kwa Mungu na Wahenga wao, huukilia mgawanyo wa majukumu kiutamaduni kwa wanajamii, na huukilia mafanikio kwa wanajamii. Kadhalika, ujinsia hudhibiti mawanda ya upataji wa maarifa kwa wanajamii, na huchochea wanajamii kuchukia lugha na tamaduni zao.

Kwa ujumla, data za makala hii zimeonesha kuwa ujinsia unaodokezwa katika majina ya watu ya jamiilugha za Kibantu umejengwa katika misingi ya mfumodume ambayo hulenga kujenga na kuimarisha utawala wa wanaume huku ikibomoa hadhi ya wanawake. Kwa mantiki hiyo, imeonekana kuwa majina ya watu na mchakato wa uteuzi wa majina hayo bado umekitwa katika mila, desturi, falsafa, na itikadi za jadi zinazomjenga na kumwendeleza mtoto wa kiume kuwa kiongozi, mtawala, mlinzi, mwenye kukidhi mahitaji ya familia, mkakamavu, na mrithi na mmiliki wa rasilimali za familia na jamii huku mtoto wa kike akifinyangwa na kuandaliwa kuwa msaidizi wa mwanaume, mlezi wa familia na mwenye kutekeleza majukumu yote ya nyumbani. Kwa ujumla, kutokana na changamoto na mabadiliko ya kimaisha yanayotokea ulimwenguni, mkakati mmojawapo wa kuleta usawa wa kijinsia unaotoa fursa sawa kwa wanajamii kushiriki katika shughuli za kijamii, kiuchumi, kisiasa, na kielimu, ni pamoja na wanajamii kuruhusu mabadiliko katika baadhi ya mila, desturi, falsafa, na itikadi zao, pamoja na uteuzi wa majina jumuishi ya watu kutoka katika lugha za asili yasiyodokeza ubaguzi wa kijinsia. Yaani, watoto (wote wa kiume na wa kike) wapatiwe majina yanayowajengea kujiamini, kuwa karibu na Mungu na wahenga, ujasiri, uadilifu, kuchapa kazi, kutafuta maarifa, kujitegemea, uongozi, kuthubutu mambo makubwa, uwezo wa kufikiri kiurazini, upambanaji, na uwezo wa kukidhi mahitaji ya familia na jamii.

## MAREJELEO


- AbdAlgane, M.(2021). Gendered Language:A Study of SociolinguisticTheories and Approaches.
- Katika *Asia ESP Journal*. Juz. 17. Na. 3.1. Kur. 204-215.
- Abdul, A. (2013). Maana na Sababu za Kiisimujamii katika Majina ya Koo za Kiluguru.
- Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Adejare. O. (1992). Language and Style in Soyinka lbadan: Heinemann Educational Books.
- Baitan, B. (2010). A Morphosemantic Analysis of Ruhaya Personal Names. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Bichwa, S.S. (2025). Language vis-a-vis Cultural Discourse: an Ethno-Pragmatic Examination of IgiHa Personal Names. Katika *Cogent Arts & Humanities*. Juz. 12. Na. 1, 2524244.
- Buberwa, A. (2018a). “Sexisim in Haya Language Personal Names Selection.” *JULACE.* 3(2): 111-126.
- (2018b). “Kiswahili Personal Names Selection in Tanzania: A Sociolinguistic Analysis.” Katika *Kiswahili*. Juz. 80, Na. 1. Kur. 21-31.
- (2022). “Changamoto katika Matumizi ya Majina ya Lugha za Kigeni nchini
- Tanzania: Mtazamo wa Nadharia ya Ubeberu wa Kiisimu.” Katika Kioo cha Lugha. Juz. 20(1): 115-129.
- Dong, J.Y. (2014). Study on Gender Differences in Language under the Sociolinguistics. Katika *Canadian Social Science*. Juz. 10. Na. 3. Kur. 92-96.
- Formato, F. na Somma, A.L. (2023). Gender Inclusive Language in Italy: A Sociolinguistic Overview. Katika *Mediterranean and European Linguistic Anthropology*. Juz. 5. Na. Kur. 22-40.
- John, S. (2016). Utaratibu wa Utoaji Majina ya Asili na Maana Zake katika Jamii ya Wamasai.
- Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Kones, N., Ali, A.H.T, na Gwachi, M. (2022). Maudhui kuhusu Jinsia katika Nyimbo za Kampeni za Kisiasa katika Kaunti ya Bomet, Nchini Kenya. Katika *Eastern Africa Journal of Kiswahili*. Juz. 01. Na. 01. Kur. 76-83.
- Lusekelo, A. na Mtenga, V. (2020). “Historicity of Personal Names in Tanzania: The Case of the Names in the Rombo-Chaga Community in Kilimanjaro.” Internatinal Journal of Modern Anthropology, Chuo Kikuu cha Dodoma.
- Madila, Z. (2020). Matumizi ya Majina ya Kiswahili Jijini Dar es Salaam, Nchini Tanzania:
- Uchunguzi Kifani wa Majina ya Watu. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- Maho, J. (2014). ‘‘A Classification of Bantu Lnguages: An Update of Guthries’s Referential
- System’’. Katika D. Nurse Na G. Philippson, (Wah). *The Bantu Languages*. London na New York: Routledge Taylor na Francis Group. Kur. 639-6641.
- Mensah, O.E. (2023). Husband is a Priority: Gender Roles, Patriarchy and the Naming of Female Children in Nigeria. Katika *Gender Issues*. Juz. 40. Kur. 44-64.
- Nyangaywa, M. (2013). Uchunguzi wa Semantiki na Taratibu za Utoaji wa Majina ya Kijita.
- Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dares Salaam.
- Pilcher, J. (2017). Names and ‘‘Doing Gender’’: How Forenmes and Surenames Contribute to Gender Identities. Katika *Sex Roles*. Juz. 77. Kur. 812-822.
- Pondelíková, I. na Štulajterová, A. (2024). Sociuolinguistic Aspects of Gender-(in)sensitive Language in English and Slovak. Katika Current Issues in Philology and Pedagogical Linguistics. Juz. 1. Na. 2. Kur. 245-252.
- Rubanza, Y.I. (2000). “The Linguistic Creativity of Haya Personal Names.” Kiswahili. 63:11-22.
- Salihu, H.H. (2014). The Sociolinguistics Study of Gender Address Patterns in the Hausa Society. Katika *International Journal of Social Science and Humanity*. Juz. 4. Na. 1. Kur. 48-53.
- Wamitila, K.W. (1999). What’s in a Name: Towards Literary Onomastics in Kiswahili Literature. Katika *AAP*. 60: 35-44.
- Wanyama, K.J.L. (2022). Uyahe na Raghba ya Jinsia kama Mikakati ya Propaganda:Uchunguzi Kifani wa Mdahalo wa Urais wa Kenya, 2013. Katika *Journal of Social Sciences, Education and Humanities.* Juz. 01. Na. 01. Kur. 89-100.
- Wappa, J.P. na Wada, R.S. (2019). Kamuə Female Personal Names and Identity in Cultural Contexts. Katika *Open Journal of Modern Linguistics.* Juz. 9. Kur. 104-114.
- Zawawi, S. (1993). *What is in Name? A Swahili Book of Name*. Triton New Jersey: The Red Sea Press.


**Cite This Article:** Madila, Z. (2026). Athari za Ujinsia Unaodokezwa katika Majina ya Watu ya Jamiilugha za Kibantu Nchini Tanzania. *East African Scholars J Edu Humanit Lit, 9*(9), 548-559. https://doi.org/10.36349/easjehl.2026.v09i09.003